# Jarida la MIUNDOMBINU YETU

TOLEO LA 02 | MAALUM LA MTANDAONI | JANUARI 2026




# “ETDCO yatia saini Mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa REA”




*#KaziNaUtu #TunasongaMbele #TabasamuLaUtu*

## Mhandisi Mwanja : Tuzingatie Ushirikiano, Uwazi na Uwajibikaji



ETDCO yashiriki Baraza Kuu la 55 la Wafanyakazi wa TANESCO




Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi, ameshuhudia Kampuni ya ETDCO ikisaini mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa REA

*Scan hii Code Kujiunga na Ukurasa wetu wa WhatsApp*

# ETDCO YASAINI MIRADI YA REA KUUNGANISHA UMEME VITONGOJI 620




Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Hatua ya Serikali kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ya kusambaza umeme katika maeneo ya vijijini imepata msukumo mpya baada ya Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umeme (ETDCO) kusaini mikataba ya kutekeleza miradi ya kuunganisha umeme katika vitongoji 620 vya Mikoa ya Katavi na Ruvuma, miradi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 95.2.

Hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo iliyofanyika Januari 17, 2026 jijini Dodoma, imekuwa kielelezo cha dhamira ya Serikali ya kuharakisha upatikanaji wa nishati ya umeme vijijini kama chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembi, amesisitiza umuhimu wa uadilifu, uwajibikaji na usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati, huku akibainisha kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kutaleta manufaa kwa wananchi.

Mhe. Ndejembi amesema upatikanaji wa umeme wa uhakika katika maeneo ya vijijini utafungua fursa mpya za kiuchumi, kuimarisha huduma za afya na elimu, pamoja na kuongeza thamani ya shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na wananchi wa maeneo husika.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa REA, Mhandisi Hassan Said, amesisitiza umuhimu wa utekelezaji wa miradi ikiwemo kuzingatia ubora, kwani mafanikio ya programu ya umeme vijijini yanategemea kiasi ya utekelezaji wa miradi kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu.

"Serikali imelenga kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya umeme ya uhakika, endelevu na yenye tija" amesema amesema Mhandisi Said.

Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya ETDCO, Mhandisi Richard Mwanja, amesema kuwa kupewa dhamana ya kutekeleza miradi hiyo ni ishara ya imani kubwa iliyojengwa kati ya kampuni na Serikali.

Mhandisi Mwanja amesema kuwa ETDCO imejipanga kikamilifu kwa rasilimali watu na vifaa ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa wakati na ubora unaokidhi matarajio kwa kuzingatia masharti ya mikataba.

Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika kwa kipindi cha miaka mitatu na itawanufaisha wananchi wa takribani 19,950 katika mikoa ya Katavi na Ruvuma.

Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 500, ikiwemo ajira za moja kwa moja, hivyo kuongeza kipato kwa wananchi na kuimarisha uchumi wa maeneo husika.

Utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha maendeleo jumuishi na endelevu. Kukamilika kwake kutachochea ukuaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi, kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini, na kuendeleza dira ya Taifa ya maendeleo ya viwanda na ustawi wa jamii.




Waziri wa Nishati, **Mhe. Deogratius Ndejembi**, ameshuhudia Kampuni ya **ETDCO** ikisaini mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa **REA** wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji 620 vya Mikoa ya Katavi na Ruvuma, wenye thamani ya shilingi bilioni 95.2 katika hafla iliyofanyika , 17 Januari 2026, Mkoani Dodoma

etdco_tz
www.etdco.co.tz

# MHANDISI MWANJA : TUZINGATIE USHIRIKIANO, UWAZI NA UWAJIBIKAJI




Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umeme (ETDCO), ambaye pia ni Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Mhandisi Richard Mwanja, amefungua Kikao cha Wafanyakazi wa ETDCO, huku akiwataka kuzingatia misingi ya ushirikiano, uwazi, uwajibikaji pamoja na ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao hicho,
kilichofanyika Januari 19, 2026 katika Ukumbi wa Mikutano wa Vizano, jijini Dodoma, Mhandisi Mwanja amesema kuwa ni muhimu wafanyakazi kuzingatia misingi ya kazi kwani ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya ETDCO na kuimarisha utendaji wa Kampuni.

Mhandisi Mwanja amesema kuwa mafanikio ya Kampuni yanategemea kwa kiasi kikubwa mchango wa kila mfanyakazi, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anatekeleza majukumu yake kwa bidii, weledi na ubora unaotakiwa, ili miradi isimamiwe na kukamilika kwa wakati uliopangwa.

Aidha, amesisitiza umuhimu wa utunzaji wa taarifa za Kampuni, kwani taarifa hizo ni rasilimali muhimu inayopaswa kushughulikiwa kwa umakini na kuzingatia maadili ya kazi.

“Utekelezaji wa majukumu kwa uadilifu, uwazi na kuzingatia sheria na taratibu ni msingi wa kujenga imani baina ya uongozi, wafanyakazi na wadau wa mbalimbali wa Kampuni” amesema Mhandisi Mwanja.

Mhandisi Mwanja amewahimiza wafanyakazi kuwa wabunifu na wenye mawazo chanya yatakayosaidia kuboresha utendaji wa Kampuni, kuongeza tija katika utekelezaji wa miradi, pamoja na kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya sekta ya nishati nchini.

Kwa upande wao, Wafanyakazi wa Kampuni ya ETDCO wameushukuru uongozi kwa kuandaa kikao hicho na kuwapa fursa ya kujadili kwa pamoja masuala mbalimbali yanayohusu ustawi wa wafanyakazi na maendeleo ya Kampuni.

Wamesema kuwa vikao vya aina hiyo vinaimarisha mshikamano, mawasiliano na uelewa wa pamoja kati ya uongozi na wafanyakazi.

Wameahidi kuendelea kushirikiana na uongozi katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na kuhakikisha ETDCO inafikia malengo iliyojipangia kwa manufaa ya Taifa.
mu.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) wakiimba wimbo wa mshikamano wakati wa kikao cha wafanyakazi kilichofanyika , Januari 19, 2026, katika Ukumbi wa Mikutano wa Vizano, jijini Dodoma.

# WAZIRI NDEJEMBI AIPONGEZA TANESCO KWA MAGEUZI MAKUBWA YA HUDUMA KWA WATEJA




Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratious Ndejembi, amelipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kuchukua hatua za kimkakati katika kuboresha huduma kwa wateja, jambo ambalo litsaidia shirika hilo kuonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na wenye ufanisi kwa wananchi.

Akizungumza Januari 22, 2026 jijini Dodoma wakati akifungua Baraza Kuu la 55 la Wafanyakazi wa TANESCO, Waziri Ndejembi amesema mabadiliko yanayotekelezwa na shirika hilo yameanza kuzaa matunda na kutoa matumaini mapya kwa wananchi, hususan katika kuboresha mawasiliano, uwajibikaji na utoaji wa huduma kwa wakati.

“Ni wazi kuwa TANESCO ipo katika mwelekeo sahihi. Mageuzi haya yanaakisi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha huduma za umeme zinakuwa bora, za kisasa na zinazomjali mwananchi,” amesema Waziri Ndejembi.

Waziri huyo ameeleza kuwa moja ya hatua muhimu zilizochukuliwa ni kuimarishwa kwa mifumo ya mawasiliano kwa wateja kupitia matumizi ya majukwaa ya kidijitali, ikiwemo WhatsApp Sogozi na mfumo wa Bulk SMS, unaowezesha shirika kuwafikia wateja wake kwa haraka pale panapotokea hitilafu au taarifa muhimu zinazohusu huduma ya umeme.

Amesema maboresho hayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza usumbufu kwa wateja na kuongeza uwazi katika utoaji wa taarifa, hatua inayojenga imani ya wananchi kwa shirika.

“Teknolojia imekuwa nyenzo muhimu katika kuboresha huduma. Kupitia mifumo hii, wateja wanapata taarifa kwa wakati, jambo linalopunguza malalamiko na kuongeza uelewa,” ameongeza.

Waziri Ndejembi amesifu uzinduzi wa namba maalum ya huduma kwa wateja ya 180, inayopatikana bila malipo, akisema hatua hiyo kupunguza upotevu wa nishati.

Vilevile, Waziri huyo ametaja mpango wa “Konekti Umeme – Pika kwa Umeme” kwa wateja na wafanyakazi wa TANESCO kuwa ni mkakati muhimu unaoendana na sera ya taifa ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, akisema mpango huo unachangia kulinda mazingira, kupunguza gharama za maisha na kuimarisha




imeongeza urahisi kwa wananchi kutoa malalamiko, kufuatilia changamoto za umeme au kupata msaada wa haraka kutoka kwa TANESCO.

Katika hatua nyingine, Waziri Ndejembi amepongeza matumizi ya mita janja (Smart Meters), akisema teknolojia hiyo imeleta mapinduzi katika usimamizi wa matumizi ya umeme, kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na kupunguza migogoro kati ya wateja na shirika.

Ameeleza kuwa mita hizo zinamwezesha mteja kufuatilia matumizi yake kwa urahisi, huku TANESCO ikiimarisha udhibiti wa mapato na afya ya jamii.

Amehimiza wafanyakazi wa TANESCO kuendelea kufanya kazi kwa weledi, uzalendo na uadilifu, akisisitiza kuwa mafanikio ya mageuzi hayo yanategemea kwa kiasi kikubwa mshikamano na uwajibikaji wao.

Kwa upande wake, Menejimenti ya TANESCO imeahidi kuendelea kutekeleza maagizo ya Serikali kwa kuongeza ubora wa huduma, kuimarisha miundombinu ya umeme na kuwekeza zaidi katika teknolojia za kisasa kwa manufaa ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla.
.




Januari 22, 2026

# **ETDCO** yashiriki Baraza Kuu la 55 la Wafanyakazi wa **TANESCO**

www.etdco.co.tz

etdco_tz

Dodoma





Pressure Cooker


Air Flyer


Rice Cooker

# UMEME NISHATI NAFUU ZAIDI JIKONI

- Huokoa muda jikoni
- Ni salama kwa matumizi
- Hulinda afya, haitoi moshi
- Hutunza mazingira
- Ni safi jikoni
- Ni gharama nafuu mno

# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YAPATA UELEWA WA MUUNDO NA MAJUKUMU YA TANESCO NA TAASISI ZAKE TANZU





*Scan hii Code Kujiunga na Ukurasa wetu wa WhatsApp*



Na Mwandishi Wetu,

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Subira Mgalu (Mb), imekutana na watendaji wa Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizo chini ya wizara hiyo katika kikao kilichofanyika tarehe 21 Januari 2026, katika Ukumbi wa Bunge, Jijini Dodoma.

Lengo la kikao hicho lilikuwa kupata uelewa kuhusu muundo na majukumu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) pamoja na kampuni zake tanzu ikiwemo Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme (ETDCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Katika kikao hicho, ETDCO iliwakilishwa na Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Mhandisi Richard Mwanja, ambaye alipata wasaa wa kuelezea majukumu ya ETDCO katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme nchini.





ETDCO

*Suluhisho la Miundombinu ya Umeme*